

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



Unapo jibuta fadhalitaja:

HM/SI/M.40/81VOL. IV/42

01 Oktoba, 2024

TANGAZO

KWA UMMA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA
KUHUSU KUFUNGULIWA KWA UTOAJI WA MIKOPO KWA
VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE
ULEMAVU.

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1) ya utoaji na usimamizi wa mikopo
ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu weny ulemavu za mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida anatangaza
kufunguliwa kwa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu weny
ulemavu na uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake,
vijana na watu weny ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi
1,101,045,729.402 zimetengwa katika robo ya 1 ya mwaka wa fedha.

2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia
ya mfumo katika Ofisi za serikali za Mitaa(Kijiji/Kata) zilizopo katika maeneo
yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu weny ulemavu
kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kwa njia
ya mfumo wa kieletroniki.
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au
wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za
ujasiriamali,


- (iii) Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenyewe ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 7 a(1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyewe ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyewe akili timamu na wenyewe umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenyewe umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambalisho vifuatavyo; Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa kijiji/mtaa kwa kuandika jina lake, saini na kugonga mhuri wa serikali ya Kijiji, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyio ndani ya mfumo wa kieletroniki na taarifa ya akaunti ya benki yenye jina la kikundi au Jina la mtu mwenye ulemavu mmoja aliyekosa wenzake wa kuungana nao

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 31 mwezi 10 mwaka 2024

Tangazo hili limetolewa na: -


Joanfaith J. Katarata
MKURUGENZI WA MANISPAA
SINGIDA 
MKURUGENZI WA MANISPAA
SINGIDA